


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI
WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI - TANZANIA
(TARURA)



TAARIFA YA UJENZI WA MRADI WA DARAJA NDONGOSI KATIKA MPAKA WA KATA YA MBANGAMAO NA KAGUGU KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDUGU CHARLES FRANCIS KABEHO TAREHE 05/06/2018

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Ninayo furaha kubwa kukuaribisha pamoja na msafara wote uliofuatana nao hapa katika Daraja la Ndongosi linaloonganisha kata mbili ambazo ni Mbangamao na Kagugu nasema karibu sana na ujisikie upo nyumbani.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Mji wa Mbinga ina miradi (mikataba) miwili inayotekelezwa kwa sasa ambayo ni miradi ya matengenezo ya barabara za mjini. Ujenzi wa Daraja la Ndongosi ambalo leo unalifungua ni miongoni mwa kazi zilizopo katika Mradi I.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Ujenzi wa Daraja hili la Ndongosi ambalo litaunganisha Kata mbili za Mbangamao na Kagugu litakuwa ni msaada mkubwa kwa wananchi wa kata hizi pamoja na Vijiji vinavyozunguka. Kufunguliwa kwa Daraja hili kutaimarisha huduma za usafirishaji kuwa bora zaidi katika kata hizi.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Mradi huu unajengwa na Mkandarasi OVANS CONSTRUCTION LTD ya Mbinga kwa gharama ya shilingi 116,188,487.60 kwa mkataba mzima. Daraja pekee ikiwa ni moja ya kazi zilizopo katika mradi huu limejengwa kwa gharama ya shilingi 20,989,320.00; Kazi hii imeanza tarehe 15/03/2018 na imekamilika 3/05/2018. Mradi huu utahudumia wakazi 1650 kwa sasa kati ya 4430 wanaotegemea kuongezeka baada ya miaka 20

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Daraja hili litasaidia usafirishaji na uendeshaji wa Shughuli mbalimbali zinazohusiana na Elimu. Kufunguliwa kwa Daraja hili kutasaidia mawasiliano wa Kata hizi mbili na

Taasisi zote za wadau wa Elimu, hivyo tunaunga mkono kauli mbiu inayosema.
“Elimu ni Ufunguo wa Maisha wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu”

Ahsante, naomba kuwasilisha.

(Eng. Ismail Mafita)
MENEJA HALMASHAURI
HALMASHAURI YAMJI-MBINGA